



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb: Na. HWC/L.20/1/VOL.1V/96/ARR

12.11.2024

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC),  
S.L.P 938,  
DAR ES SALAAM.**

**YAH: ENEO LA ARDHI YA MWEKEZAJI NINE HILLS TANZANIA LIMITED KATIKA  
KIJIJI CHA CHAMAKWEZA CHALINZE**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Tunapenda kukutaarifu kuwa tarehe **23.10.2024** ofisi ilipokea barua kutoka kwa Nine hills Tanzania Limited iliyopitishwa na Mtendaji wa Kijiji Cha Chamakweza wakiomba kupimiwa eneo lao la ekari mia mbili zinazopatikana katika kitongoji cha **Njiapanda**.

Kampuni tajwa hapo juu wameonesha nia ya kuwekeza katika kijiji hicho kuanzisha ufugaji wa kuku (Poultry Farming).

Kampuni ya **Nine Hills Tanzania Limited** ilipata eneo hilo kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao **sita (6)** katika kijiji cha Chamakweza. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kupipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji tarehe **18/10/2024** na mapendekezo ya kikao cha Halmashauri ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Chamakweza uliofanyika tarehe **18.10.2024** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114**, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa **ekari 200** ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

- (a) Mwekezaji kutoa kipaumbele kwa ajira zitakazopatikana katika kijiji hicho
- (b) Mwekezaji kuchangia maendeleo ya kijiji

Kwa kuwa ukomo wa ugawaji ardhi ngazi za Halmashauri ya kijiji ni ekari 50; Halmashauri ya Wilaya ilipokea muhtasari wa kijiji ukipendekeza kummilikisha mwekezaji **Nine Hills Tanzania Limited** kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 18/10/2024 na kubaini yafuatayo:

- (a) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekari 200
- (b) Eneo hilo halijafanyiwa maendeleo yoyote

**Kwa sababu hizo, tunapenda kudhibitisha kuwa eneo hilo ni mali ya Kampuni Nine Hills Tanzania Limited ambayo imenunua kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao sita wenye jumla ya ekari mia mbili (ekari 200).**

**Pili tunadhhibitisha kuwa tarehe 18.10.2024 ofisi ilifika eneo hilo na haikubaini mgogoro wowote wakati wa ukakaguzi.**

Pamoja na barua hii, nimeambatisha mikataba ya manunuzi, muhtasari ya vikao vyote viwili vilivyoadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria.

Naomba kuwasilisha taarifa hii ili uwe kwenye nafasi nzuri kutoa "certificate of incentive" ya kwa hatua zinazofuata.



Ramadhani Possi  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
CHALINZE**



**Nakala kwa: NINE HILLS TANZANIA LIMITED**

**S.L.P 21234,**

**DAR ES SALAAM (kwa taarifa na ufuatiliaji).**

**Mtendaji wa Kijiji Cha Chamakweza (kwa taarifa)**